



JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA
NA
SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA
NACHINGWEA



Unapojibu Tafadhali taja:

Kumb. Na.LA.142/219/5

Tarehe: 15/04/2025

Mkurugenzi Mtendaji,
Kituo Cha Uwekezaji Tanzania (TIC),
SLP 938,
DAR ES SALAAM.

**YAH: UTAMBULISHO WA KAMPUNI YA VILLAGE CLIMATE SOLUTIONS
LIMITED (VCSL)**

Rejea somo tajwa hapo juu.


1. Naitambulisha kwako kampuni tajwa hapo juu, ambayo ina malengo ya kuwezesha vijiji vya Wilaya ya Nachingwea kutekeleza biashara ya Kaboni kupitia mfumo unaojulikana kama "Mkakati wa Kupunguza Uzalishaji wa Hewa Ukaa inayotokana na ukataji miti hovyona uharibifu wa misitu" (MKUHUMI).
2. Mpango huu unasaidia utunzaji wa Misitu ya Asili inayomilikiwa na Vijiji, kwa mujibu wa Vifungu namba 4 (c) (i), 32 (1) (a) na (b) na 35 (6) (b) vya Sheria ya Misitu sura ya 323 ya Sheria za Tanzania.
3. VCSL inashirikiana na vijiji na Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea kutekeleza MKUHUMI, kwa lengo la kuzalisha na kuuza kredit za Kaboni, ambapo vijiji vitapata fedha zitakazosaidia maendeleo ya jamii hususani kuboresha kilimo, afya, maji na upatikanaji wa hati miliki za ardhi.
4. Mradi wa VCSL inajulikana kama *Village Climate Solutions Project (VCSP)* na imepitishwa na Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea kwa kuridhiwa na mikutano mikuu ya vijiji 16 pamoja na baraza la madiwani na baadae kuendelea na taratibu za usajili katika Ofisi ya Makamu wa Rais na Mfumo wa Kimataifa wa Viwango vya Kaboni na Viwango vya Ubora.
5. Katika Wilaya yetu, Mradi huu unatekelezwa katika vijiji vya Matekwe, Majengo, Majonanga, Kilimarondo, Nanjihi, Namatunu, Kiegei "B", Kiegei "A", Nahimba, Mbondo, Chimbendenga, Nakalonji, Mtua, Lionja "B", Ngunichile na Lipuyu.

6. Tunawaomba Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kitambue uwepo wa kampuni hii na kutoa ushirikiano zaidi kwa kampuni hii ili kuhakikisha taratibu za uwekezaji katika utekelezaji wa mradi huu zinafuatwa ili kuhakikisha upatikanaji wa manufaa kwa jamii.
7. Natanguliza shukrani.




Dr. Ramadhani N. Mahiga
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
NACHINGWEA

MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAUMI YA WILAYA
NACHINGWEA



Nachingwea Kaskazini



Nachingwea Kusini